**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SINGIDA**

SHULE YA SEKONDARI MAGHOJOA,
S.L.P 1029,
**SINGIDA.**
**Tarehe……………...**

Namba za simu
MKUU WA SHULE: 0764451747
MAKAMU MKUU WA SHULE: 0756320444
MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI……………………………………………………………………..
S.L.P…………………………………………………………………………………………………

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO (V) MWAKA………………KATIKA SHULE YA SEKONDARI MAGHOJOA:**

1. Ninafurahi kukuarifu kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano Tahasusi ya HGE, EGM katika Shule ya Sekondari MAGHOJOA iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Mkoa wa Singida, Hongera sana.
   Shule ipo umbali wa Km 42 kaskazini mwa mji wa Singida, Shule hii ni ya mchanganyiko kwa Kidato cha I hadi IV na wavulana tu kwa kidato cha V na VI.
   Usafiri wa kufika shuleni ni wa magari madogo ya abiria aina ya Noah ama Coster. Wanafunzi wanaotoka nje ya mkoa wa Singida, watashuka stendi kuu ya mabasi Misuna, na kupanda bajaji au bodaboda hadi stendi ya Msufini,hapo utapanda Noah zinazoenda Maghojoa, magari huondoka mjini singida kuanzia saa 12:30 asubuhi hadi saa 12:00 jioni kila siku, nauli yake ni shilingi elfu tano (5000/=) na kituo cha kushukia ni shuleni moja kwa moja yaani - Shule ya Sekondari Maghojoa.
   Muhula wa masomo utaanza kwa tangazo la Serikali Mwanafunzi anatakiwa kuripoti Shuleni. Kama una matatizo yatakayokuzuia kufika mapema Shuleni toa taarifa mapema, vinginevyo unaweza kupoteza nafasi yako. Unapofika Shuleni hakikisha kuwa unaleta mahitaji yote yaliyoelekezwa na kuambatanishwa na barua hii. Aidha, Wanafuzni watakaokuwa wanalipiwa ada na mamlaka mbalimbali za sehemu wanazotoka kwa mfumo wa Serikali kuu, Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa, Jiji, Vijiji au Wafadhili, Shule

inaomba barua za mamlaka hizo zikielezea namna watakavyolipa na lini ili wasikwamishe uendeshaji wa shughuli za Shule.

## 2. MAMBO YA KUZINGATIA:

### 2.1 ADA NA MICHANGO MINGINE YA SHULE

(i) Mchango wa uendeshaji wa shule 65,000/=

(ii) Nembo ya shule 5,000/=

(iii) Tahadhari Tsh. **5,000/=(** unalipa yote, haitarejeshwa)

(iv) Kitambulisho Tsh. **5,000/=**

**Jumla ni Shilingi 80,000**

**NB.** Fedha hizi ziwekwe kwenye Akaunti ya Shule **Na.50801100145** jina la Akaunti ni **Maghojoa Secondary school** Benki ya **NMB**. Original bank pay in slip ipelekwe kwa Mhasibu wa Shule (Hakikisha bank pay in slip ina jina la Mwanafunzi,kidato na orodha ya vitu ulivyolipia nyuma yake). Kama hauna kadi ya Bima ya Afya uje na Tsh. **50,400/=** kwa mwaka kwa ajili ya kukatia Bima ya Afya. Ni kwa wale wasio na Bima za afya.

### 2.2 SARE ZA SHULE

(i) Suruali 2 rangi ya khaki za kitambaa, ziwe na mifuko mitatu na marinda mawili, mishono ya heshima (sio mtepesho) na zisiwe "jeans style" au za kubana (MODO)

(ii) Mashati 2 ya mikono mirefu meupe (tetron) yasiyo na nakshi yoyote.

(iii) Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba, visivyo na visigino virefu

(iv) Soksi nyeusi jozi mbili au zaidi

(v) Sweta la mikono mirefu rangi ya Kijani kibichi

(vi) Tai ndefu rangi ya Kijani yenye mistari meupe

(vii) T-shirt 2 rangi ya bluu Bahari na zinapatikana shuleni

### 2.3 NGUO/SARE ZA MICHEZO NA KAZI

(i) Bukta na T-shirt rangi ya bluu kwa ajili ya michezo

(ii) T-shirt ya rangi ya damu ya mzee na Suruali nyeusi kwa ajili ya kazi za nje.

(iii) Raba nyeusi ya kuvaa wakati wa michezo, kazi na wakati wa masomo ya jioni.

(iv) Tracksuit ya bluu au bluu bahari au nyekundu

### 2.4 MAHITAJI YA BWENI

(i) Shuka mbili rangi ya pinki au bluu

(ii) Godoro la (unene) nchi $2^{1/}{}_{2,}$ urefu futi 6 na upana futi $2^{1/}{}_{2}$

(iii) Chandarua

(iv) Blanketi

(v) Taulo

(vi) Kitana,sabuni za kuogea na kufulia

(vii) Ndoo ya plastiki lita 10 au 20 kwa ajili ya kuogea na kufulia ziwe mbili (02)

(viii) Dumu/ndoo ya lita 10 yenye mfuniko kwa ajili ya maji ya kunywa

(ix) Vifaa vya chakula (sahani,bakuli,kikombe na kijiko)

(x) Taa ndogo ya Solar (kwa dharura umeme ukikatika-muhimu sana) mishumaa haitakiwi

2.5 **VIFAA VYA USAFI**

(i) Ufagio1 (soft broom) kwa usafi wa ndani na Chelewa 1 kwa ajili ya usafi wa nj(HGE/EGM)

(ii) Mopa/ squeezer(HGE/EGM)

(iii) Jembe jipya 1 (HGE/EGM)

(iv) Panga (EGM)

(v) Kwanja (HGE)

2.6 **VIFAA VYA KUJIFUNZIA**

(i) Madaftari makubwa 12 (counter books Q3 au Q4)

(ii) Rim 1 ya karatasi A4

(iii) Rim 1 ya karatasi (ruled paper)

(iv) Mathematical set moja

(v) Kalamu ya wino,penseli na ruler

(vi) Advanced learner's Dictionary

(vii) Vitabu vya tahasusi – HGE/EGM

(viii) Jalada (file) mbili kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za Mwanafunzi

(ix) Scientific calculator moja

**3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1987 na kama iliyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Raisi-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Hivyo unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

(a) Heshima kwa viongozi,wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya Shule kulingana na ratiba ya Shule ni lazima.
(c) Kushiriki kwa umakini kufanya maandalio ya jioni (kujisomea) ukiwa Shuleni ama nyumbani.
(d) Kuwahi katika kila shughuli za Shule na zinginezo utakazopewa
(e) Kufahamu mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote ukiwa mwanafuzni katika Shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya Shule.
(g) Kuvaa sare ya Shule wakati wote unaotakiwa
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
(i) Kutunza mali za Umma
(j) Huruhusiwi kunyoa kipara, kufuga nywele ndefu, kufuga kucha ndefu, kupaka rangi midomo na kucha, kutinda nyusi, kupaka wanja, kuvaa heleni, bangili, mikufu, nguo fupi na nguo zisizo na heshima na adabu.
(k) Mwanafunzi haruhusiwi kuja na simu au laini yoyote ya simu Shuleni.

**4. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.**

(a) Wizi
(b) Uasherati na ushoga
(c) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi na kadharika
(d) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, au mwanafunzi kumpiga mwalimu au mtu yoyote Yule
(e) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
(f) Kudharau Bendera ya Taifa
(g) Kusababisha mimba
(h) Kuoa
(i) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa Shule na watu
(j) Kukataa adhabu kwa makusudi
(k) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu katika mazingira ya Shule
(l) Utoro wa kuwa nje ya eneo la Shule bila ruhusa
(m) Kulala nje ya Shule Mwanafunzi wa Bweni bila ruhusa
(n) Kuwa Bwenini muda wa masomo bila ruhusa
(o) Kutohudhuria darasani, kujisomea wakati wa jioni (preparation time)
(p) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria
(q) Kutoa lugha chafu kwa mwalimu, wanafunzi wenzako, walezi, na jamii kwa ujumla
(r) Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kunywa sumu n.k
(s) Kumdharau mwalimu, kiongozi, mfanyakazi na jamii kwa ujumla
(t) Kutohudhuria vipindi kwa uzembe na kutofanya mitihani au majaribio kwa makusudi.

## NB: SIMU HAZIRUHUSIWI SHULENI.

**PRIME MINISTER'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**SINGIDA DISTRICT COUNCIL**
**MAGHOJOA SECONDARY SCHOOL**

# MEDICAL EXAMINATION FORM

(To be completed by Medical Officer in respect of all new students)

Full name……………………………………………………..Age…………………………….

1. Blood count (red and white)……………………………………………………………………

2. Urine examination………………………………………………………………………………

3. Stool examination………………………………………………………………………………

4. Syphilis……………………………………………………………………………………………

5. T.B test……………………………………………………………………………………………

6. Ear test ……………………………………………………………………………………………

7. Eye test……………………………………………………………………………………………

8. Spleen……………………………………………………………………………………………

9. Abdomen…………………………………………………………………………………………

10. Additional information or any other physical, mental, hereditary of infectious diseases…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

Treatment after examination……………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………….. (MEDICAL CERTIFICATE)I certificate that the above concerned has been examined and found fit into pursue for further education.

**Signature……………………………….Designation……………………Station…………**

(Official Stamp) Date:………………………………………..

***NB: Fomu hii ijazwe na Mganga katika Hospitali inayotambulika na Serikali.***

# FOMU YA MAPOKEZI

# FOMU HII IJAZWE NA KUREJESHWA NI MUHIMU KUKAMILISHA

Picha ya Mwanafunzi

**(A) IJAZWE NA MWANAFUNZI**

**1.** Jina laMwanafunzi…………………………………2. Taifa…………….………3. Raia…………
4. Dini……………………………5. Tarehe ya kuzaliwa……………………6. Shule ya Sekondari uliyotoka………………………………………………7.Tarehe ya kutoka Shule hiyo……………………… saini ya Mwanafunzi…………………Tarehe…………………………..

Picha ya Mzazi/Mlezi

**(B) IJAZWE NA MZAZI/MLEZI**

1. Jina la Mzazi/Mlezi…………………………………………2. Anuani kamili……………………
2. Sehemu unapoishiMtaa/Kijiji…………………………Jina la Mwenyekiti wa Serikaliya Mtaa/Kijiji………..........Kata………………………Wilaya………………Mkoa………………Namba ya Nyumba…………………………4. Namba ya simu, Ofisini au Nyumbani……………………… au jirani…………………………5. Maelezo ya kikazi: - Kazi ya Mzazi/Mlezi……………………………Jina laMwajiri…………………Idara…………………...Mahali ilipo……………………Anuani……………………Namba ya simu…………………

**S**aini ya Mzazi/Mlezi………………………… Tarehe……………………………….

**AHADI YA MZAZI/MLEZ**I

Mimi ………………………………… Mzazi/Mlezi wa………………………………………ambaye amechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika Shule ya Sekondari Maghojoa mwaka 2026.Ninaahidi kulipa ada na michango ya Shule kwa wakati,pia nakiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo yaliyotolewa na Shule ya Sekondari ya Maghojoa, Nimeyasoma na kuyaelewa kikamilifu. Ninaahidi kuyasimamia ili mtoto wangu ayatekeleze kwa ukamilifu.

Jina……………………………………………………………………………………..

Saini……………………Tarehe………………Namba ya simu……………………………

**AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi…………………………………… Mwanafunzi wa Shule ya…………………………………ambaye nimechaguliwa kujiunga na kidato cha tano (v) katika Shule ya Sekondari Maghojoa mwaka…………………, nakiri kukubaliana na sheria,kanuni na maelekezo yaliyotolewa na Shule ya Sekondari Maghojoa, nimeyasoma na kuyaelewa kikamilifu na ninaahidi kusoma kwa bidii na kufaulu masomo yote.

Jina……………………………………………Saini……………………Tarehe……… Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi………………………

**5. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**

(a). Medical examination forms ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara Mwanafunzi atakapo ripoti Shuleni

(b). Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya Mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai

(c). Fomu ya Mzazi kukiri kukubaliana na sheria,kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na Shule

(d). Picha nne za Wazazi na ndugu wa karibu wanaoweza kuja kumtembelea Shuleni na namba zao za simu

(e). Cheti halisi cha kuzaliwa na kivuli chake

(f). Nakala halisi ya matokeo ya kidato cha nne (statement of results) na kivuli chake

Tafadhali soma kwa makini maelekezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.**

**…………………………..**

**ALBERTO P. SANKA**

**MKUU WA SHULE**

**NB:** Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mtandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI AU MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO

MKUU WA SHULE: 0764451747

MAKAMU MKUU WA SHULE: 0756320444

MWANDAMIZI TAALUMA: 0756590861

MWANDAMIZI MALEZI: 0770744950